# HALI YA KISWAHILI KATIKA ELIMU NCHINI RWANDA

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY
2005/65555

NA

THADDEE R. KIMENYI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA "MASTERS OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA EGERTON

2003

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kingine chochote.

________________________ Tarehe 05/01/2003

Thaddee R. Kimenyi
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu.

________________________

Dr. S.K. Bejah Tarehe 9/01/03

________________________

Profesa Rocha Chimerah Tarehe 7th JAN. 2003

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

# TABARUKU

Kwa heshima ya mke wangu Bi.Mkayiramga Veneranda Kimenyi, na watoto wangu,
Kimenyi Monique, Kimenyi Emmanuel, Kimenyi Grace, Kimenyi Aline na Kimenyi Aime.

# YALIYOMO

SURA YA KWANZA 1

**Misingi ya Utafiti** 1

1.0 Utangulizi 1
1.1 Upeo Wa Utafiti 1
1.2 Tatizo la Utafiti 2
1.3 Madhumuni ya Utafiti 2
1.4 Nadharia Tete 2
1.5 Sababu Za Kuchagua Mada 2
1.6 Msingi wa Nadharia 3
1.7 Mapitio ya Mandishi 4
1.8 Mbinu za Utafiti 6
1.9 Ukusanyaji na Uchanganuzi wa data 7
1.10 Eneo la Utafiti 7

SURA YA PILI 8

**Historia ya Kiswahili nchini Rwanda na Afrika ya Mashariki na ya Kati** 8

2.0 Utangulizi 8
2.1 Historia fupi ya lugha ya Kiswahili Nchini Rwanda 8
2.2. Lugha ya Kiswahili Wakati wa Utawala wa Wajerumani 11
2.3 Kiswahili Nchini Rwanda 15
2.4 Kiswahili Nchini Rwanda Baada ya Mauaji ya 1994 15
2.5 Hitimisho 16
2.6 Afrika ya Mashariki na ya Kati 17
2.7 Historia Fupi ya Kiswahili Nchini Congo 19
2.8 Kiswahili Nchini Burundi 21
2.9 Kiswahili Nchini Tanzania 22
2.10 Kiswahili Nchini Kenya 27
2.11 Kiswahili Nchini Uganda 29
2.12 Hitimisho 32

SURA YA TATU 33

3.0 **Hali ya Kiswahili katika Mfumo wa Elimu Rwanda** 33
3.1 Hali ya Kiswahili Katika Elimu 36
3.2 Kuhusu Walimu wa Kiswahili 37
3.3 Kuhusu Vifaa Vya Walimu na Wanafunzi 38
3.4 Kuhusu Mazingira 40

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

SURA YA NNE 47
4.0 **Hitimisho na Mapendekezo** 47
4.1 Utangulizi 47
4.2 Pendekezo la Kwanza 48
4.3 Pendekezo la Pili 49
4.4 Hitimisho 50
Kiambatisho 51
Marejeleo 53

# SHUKRANI

Nigependa kutoa shukrani zangu nyingi kwa wasimamizi wa kazi hii Dr. Bejah Karisa na Profesa Rocha Chimerah kwa kuiongoza na kunielekeza.

Shukrani nyingi ziwaendee wahadhiri wa Idara ya Kiswahili na hasa mkuu wa Idara, Dr. Catherine Kitetu na walimu, Dr. Bejah, Bw. Mayaka Gwachi, Bw. David Chacha, wanasthili pongezi kwa mihadhara na mijadala tuliyokuwa nayo nje na ndani ya darasa.

Shukrani nyingi pia ziwaendee wanafunzi wenzangu mabwana D. Bowen na P.M. Ngugi kwa ushirikiano wao.

Mwisho ninamshukuru Bi. Jane Kabergei kwa kunipigia chapa kazi hii.

# SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

## 1.0. Utangulizi

Utafiti huu ulijishughulisha na kuchunguza hali ya lugha ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda. Utafiti ulishughulikia zaidi vipingamizi vinavyokwamiza uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda. Hii haina maana kwamba wananchi wa Rwanda hawazungumzi wala kupenda lugha hii. La hasha. Kinyume chake, lugha hii iliingizwa nchini Rwanda zaidi ya miaka mia moja iliyopita. Hakika kabisa "Kiswahili kiliingia nchini Rwanda kwa mara ya kwanza mwishoni mwa karne ya 19 kati ya tarehe 11 na tarehe 15 Disemba 1892" (Ntawigira.1997).

Matumizi ya Kiswahili nchini Rwanda siyo makubwa ukilinganisha na nchi jirani za Afrika Mashariki na hata zile za Afrika ya Kati kama vile Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kiswahili kinachozungumzwa nchini Rwanda kwa wingi ni Kingwana, lahaja ya Kiswahili inayotumiwa RDC husasan masahriki mwa nchi ya Congo (Chimerah, 2000).

Swali muhimu la utafiti huu ilikuwa ni kuona ni kwa nini Kiswahili katika elimu nchini Rwanda hakitumiwi vilivyo ilhali ndiyo lugha ngeni ya kwanza kufika Rwanda kwa muda wa zaidi ya miaka mia moja iliyopita (Karangira 1986:118)

## 1.1 UPEO WA UTAFITI

Maenezi na maendeleo ya lugha huchukua sehemu kubwa ya historia ya lugha tangu chimbuko mpaka maendeleo na maenezi yake.

Hata hivyo, kwa ajili ya wakati mdogo pamoja na kubanwa kifedha, utafiti huu ulijikita katika kutafuta zile sababu muhimu zinazoathiri uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda.

Haya yote yalitokea nchini Rwanda, lakini tuliweza kutalii uendelezaji wa Kiswahili katika nchi majirani ili tulinganishe hali zote tofauti kuhusu uendelezaji wao wa lugha ya Kiswahili katika elimu.

## 1.2.TATIZO LA UTAFITI

Kiswahili nchini Rwanda hakijaendelezwa, kama ilivyotarajiwa, katika elimu. Kama nilivyotanguliza kusema hapo juu, Kiswahili kiliingia nchini Rwanda miaka mia moja iliyopita, lakini lugha hii haijapiga hatua kimaendeleo ipasavyo nchini Rwanda. Kwa hivyo somo langu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza sababu zinazoathiri uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda.

## 1.3. MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti huu, tuliazimia;

i) Kuchunguza matatizo yanayoathiri uendelezaji wa Kiswahili katika elimu nchini Rwanda

ii) Kupendekeza hatua za kufuatwa ili kuendeleza Kiswahili katika elimu nchini Rwanda.

## 1.4. NADHARIA TETE

i) Hali ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda hairidhishi.

ii) Hali hii inaweza kuondolewa kwa kufuata mapendekezo yatakayo-tolewa.

## 1.5. SABABU ZA KUCHAGUA MADA

i) Kiswahili ni lugha mashuhuri katika nchi za Afrika Mashariki na ya Kati eneo ambalo nchi ya Rwanda nimojawapo. Hali hii ndiyo ilioyonishawishi kufanya utafiti huu, ili nihimize uendelezaji wa Kiswahili mashuleni

ii) Matokeo ya utafiti yatawanufaisha wasimamizi wa sera ya lugha katika elimu nchini Rwanda.

## 1.6. MSINGI WA NADHARIA

Somo hili la utafiti lilifanyika kwa nguzo za "Mpango wa lugha" (language planning) kama alivyofikiria Haugen (1966). Na haya yameèlezwa na watu kama Bokamba (1995) pamoja na Bangbose (1991). Nadharia husaidia kutoa hatua nne muhimu katika mpango wa lugha kwenye nchi husika. Hatua hizo ni kama zifuatazo.

i) Hatua ya kwanza ni ile ya kuchagua lugha moja kutoka kwa lugha nyingine zilizopo. Kutokana na mapendekezo ya mfano kama huu. Hii imefanyika baada ya kuzingatia mambo muhimu kama vile wazungumzaji wa lugha hiyo, vilevile na muundo wa lugha hiyo.

ii) Pili, usanifishaji wa lugha au lahaja iliyokubalika au kuchaguliwa katika hali ya msamiati wake, sintaksia, fonolojia, na vilevile semantiki au maana. Hii ni kuona kwamba lugha inajitosheleza kama lugha ya mawasiliano.

iii) Hatua ya tatu ni kutekeleza maenezi na matumizi ya lugha sanifu. Lugha hii sanifu inatumiwa katika kuieneza kwenye sehemu mbalimbali muhimu kama vile katika elimu, taarifa ya habari na magazeti.

iv) Sehemu ya nne ni kuona kuwa lugha inapanuliwa na kuingizwa katika mambo ya kisayansi na tekinolojia. Sifa muhimu katika nadharia hii, na yenye maana, ni pamoja na kufanya matayarisho ya hatua zilizotajwa katika uchunguzi wa lugha, maendeleo na maenezi ya lugha hiyo.

Maendeleo ya lugha; hutegemea sera ya pamoja na mikakati ya siasa kuelekea upanuzi wa lugha. Kwa kuwa utekelezaji huu ukiwa ni mzuri huinua siyo lugha sanifu tu bali hata lugha nyingine zizumgumzwapo nchini.

Kuhusu utekelezaji uliozungumziwa katika sehemu hii ya tatu na ya nne, huendelezwa na serikali, kamati za serikali au wataalamu katika vyuo, vyama vya wataalamu au vyama vya lugha. Kwa mfano, nchini Tanzania, sera ya Kiswahili hutekelezwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ambayo hufanya utafiti, upanuzi wa msamiati, uchapishaji. Kamati za Kiswahili za taasisi ya elimu zinahusika na mipango ya mtaala (Curriculum). Halmashauri ya Kiswahili ya kitaifa inahusika na kupanga maendeleo ya Kiswahili katika ngazi ya kitaifa. Halmashauri za wizara mbalimbali inahusika na maendeleo ya istilahi za kutumika katika utawala na halmashauri ya waandishi. UKUTA inahusika na maendeleo ya upande wa fasihi na utamaduni wa lugha. Kwa jumla, kuna afisi ya mwendelezaji (promoter) wa Kiswahili ambaye jukumu lake ni kuendeleza Kiswahili. Hali hii haijafanyika nchini Rwanda. Kwa hivyo utafiti huu utajikita katika kuchunguza mambo yanayotinga hatua za tatu na nne zinazopendekezwa katika nadharia ya mpango wa lugha.

## 1.7 MAPITIO YA MANDISHI

Kama vile kisio linavyosema, sababu zinazokwamiza undelezaji wa lugha ya Kiswahili ni za kijamii na kihistoria. Kufuatana na tarifa tulionayo, maendeleo na maenezi ya lugha ya Kiswahili za kijamii na kihistoria. Kufuatana na taifa tulionayo, Maendeleo na maenezi ya lugha ya Kiswahili imeanza ukinzani wakati wa watawala wa Kibelgiji(1916). Wakati wajerumani walikuwa wamekusudia kuanzisha na kueneza lugha ya Kiswahili, Wabelgiji nao walipinga jambo hilo. "Mnamo mwaka wa 1929 Kiswahili kilifutwa kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na zile za upili (Ntawigira 1997:51). Utawala wa kizungu wa Uibelgiji ulipiga marufuku lugha ya Kiswahili mashuleni. Kuhusu jambo hili tuna maelezo yafuatayo; "Mnamo mwaka 1929 mkaguzi wa ufundishaji wa kikoloni kutoka Leopoldville (Kinshasa) alisema kwamba hakukuwepo fursa ya kuendelea kutawala kwa kutumia Kiswahili. Huyo alikuwa mtumishi wa koloni za kiblegiji ndiyo sababu hoja yake ilikuwa ya kisiasa. Tangu siku hiyo, serikali ilianza kufundishia mashuleni lugha moja kati ya lugha zake rasmi zilizotumiwa na Ubelgiji (Niyibizi 1980:26).

Wakati huo mtu yeyote yule aliyekuwa na kazi katika ngazi za serikali ya wabelgiji alilazimishwa kutumia Kifaransa badala ya Kiswahili. Ndiyo sababu watumishi wa serikali ya wabelgiji waliacha lugha ya Kiswahili. Kiswahili kiliendelea kutumiwa na watu wasio na kazi za serikali kama vile wafanya biashara na wanadini haswa ya kiislamu, na watu wengine wasio na mategemeo kwa utawala wa wabelgiji. Baadaye Kiswahili badala ya kuwa na sifa ya uungwana kilibaki kuwa sifa ya ujinga.

Jinsi lugha ya Kifaransa ilivyoenea nchini Rwanda na kuwa lugha fahari, ndivyo lugha ya Kiswahili ilivyozorota na kudunishwa. Hali hiyo iliendelea mpaka mwaka wa 1962. Ingawa lugha hiyo imepigwa vita na watawala wapya, haikudidimia kabisa. Lugha ya Kiswahili imejizatiti hasa kwa kutumiwa na watu wa kawaida hasa wale waliokuwa wakifika nchini Tanganyika kwa kufanya vibarua, hawa wote walirudi wakizugnumza Kiswahili. Pia kama ilivyosemwa hapo juu, wafuasi wa dini mbalimbali kama vile waislamu, waprotestanti na waadvantisti, wachimba mgodi, na wanajeshi kutoka Congo walitumia Kiswahili na kukifanya kukabili mazingira magumu ya kukifanya kutoweka nchini Rwanda. Nyanja hizo ziliendeleza Kiswahili mbaka baada ya uhuru kufikia wakati mpya wa kushughulikiwa na serikali ya Rwanda mwaka 1977.(Ntawigira 1997).

Tangu mwaka 1962, viongozi wapya wa Rwanda walikuwa na mipango mipya ya kuendeleza nchi. Pengine inaeleweka wazi kwamba kuna athari za ukoloni zilizoendelezwa na viongozi hao, kama kuchukua lugha ya Kifaransa kama lugha kubwa kuliko nyingine na kuendelea kuwa na maoni mabovu kuhusu lugha ya Kiswahili.

Ntawigira anaendelea kutuelezea kuwa ni mnamo mwaka 1963 ndipo Kiswahili kilianza kufufuka katika shughuli za serikali. Mwaka huo ndipo Redio Rwanda ilipoanza kupeperusha matangazo ya lugha ya Kiswahili kama anavyosema, Barengayabo (1992) "Mathalani, Pindi Redio Rwanda ilipozinduliwa, kifaransa kilipewa nafasi kubwa kwa ajili ya kuwasiliana wazungumzaji wa lugha hii, hasa

wakoloni. Katika lengo la kuendeleza uhusiano huu kimkoa, matangazo ya Kiswahili yalianza kupeperushwa hewani tangu mwaka 1963".

Baada ya uhuru, Rwanda ilikuwa na lengo la kupanuwa uhusiano wake na nchi jirani. Ofisi za ubalozi zilifunguliwa mjini Kigali: Kenya na Tanzania na nchi nyingine. Redio Rwanda ilitumia Kiswahili kwa ajili ya kujiunga na Afrika ya Mashariki na nchi nyingine zinazotumia Kiswahili.

Mwaka wa 1979 ulileta mabadiliko katika mfumo mashuleni. Kiswahili kiliingia mashuleni ingawa kabla ya tarehe hiyo kilipatikana katika shule ya sayansi jamii itwayo KARURANDA na I.P.N. Baada ya mwaka huo Kiswahili kilifundishwa katika mikondo tofauti ya shule za sekondari. Kiswahili kilisambazwa mahali pote mpaka kwa shule zinazotayarisha vijana kuwa mapadri seminari ndogo na kubwa. Idara ya lugha na fasihi za Kiafrika katika chuo kikuu cha Rwanda ilianzisha masomo ya Kiswahili kwa wanachuo katika idara hiyo. Waalimu wengi kutoka Afrika ya mashariki walifika nchini Rwanda kwa ajili ya kufundisha Kiswahili (Ntawigira1997).

Nyanja mbalimbali za kibinafsi zilijaribu kukuza lugha hii; kwa mfano waislamu walijenga shule na misikiti. Wanafunzi, na wafanyakazi waliojiunga nao hawana budi waongee na kukimudu Kiswahili. Biashara ya ndani na nje ya nchi ilishughulikia sana lugha hii. Wafanya biashara wakubwa walishirikiana na wahindi na waarabu ambao lugha yao ya mawasiliano ilikuwa ni ya Kiswahili.

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mahojiano kukusanya data.Wahojiwa waliteuliwa kutoka sehemu fulani fulani katika ofisi inayosimamia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini kote Rwanda.

i) Tasisi ya uchunguzi wa masomo shule za sekondari
ii) Walimu wa shule zinazofundisha somo la Kiswahili

## 1.9 UKUSANYAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

Kama ilivyotajwa hapo juu, utafiti huu ulitumia mahojiano kukusanya data kutoka kwa wahojiwa. Sampuli ya maswali yatakayotumiwa ni kama inavyoonyeshwa katika (Kiambatisho), kwa mfano;

i) Kumuliza mhusika au wahusika wakuu wa Taasisi ya ukuzaji mitaala mpango wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kazi hiyo inavyofanyika

ii) Kuwaomba maafisa wa Tasisi ya ukuzaji mitaala ratiba ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda

iii) Kuwauliza maafisa matatizo yanayowapata walimu wa Kiswahili katika ufundishaji.

iv) Kuwaomba wakuu wa Taasisi ya ukuzaji mitaala wataje pendekezo kuhusu Kiswahili katika elimu nchini Rwanda.(tazama mwongozo wa maswali ya utafiti kwenye kiambatisho)

## 1.10 ENEO LA UTAFITI

Kama sehemu nzuri ya wahojiwa inavyo onyesha, utafiti huu ulifanyiwa sehemu moja muhimu nayo ni:

Mjini Kigali ambako kuna makao makuu ya ofisi za kusimamia ufundishaji wa masomo shuleni.

## SURA YA PILI

## HISTORIA YA KISWAHILI NCHINI RWANDA NA AFRIKA YA MASHARIKI NA YA KATI

### 2.0 UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ya Kiafrika ambayo ni maarufu sana humu Afrika na nje ya bara la Afrika. Asili ya lugha hii ni Afrika ya Mashariki sehemu za Mwambao na upwa wake.

Ijapo Kiswahili ni lugha ya wazawa wa Afrika, lugha hii imeletwa na kusambazwa na watawala wa Kijerumaini; na Wazungu ambao wameleta ukoloni nchini Rwanda mnamo karne ya 19 kama tutakavyoona katika sura hii.

Sura hii itaelezea kwa ufupi kuja mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili, lugha ambayo ilikuwa ngeni kwa jamii ya Wanyarwanda. Lugha ya Kiswahili haikuletwa na wakoloni peke yake bali waliambatana na msafara wa wafanyakazi wa Kiafrika ambao ndio waliosambaza Kiswahili. Inasemekana kwamba wapagazi hawa, pamoja na askari Waafrika, hawakupendwa na wenyeji kw sababu ya kupeleka habari kwa mabawana zao.

Pia watawala hawa walifuatana na wamishenari ambao walienea kote nchini wakitumia lugha ya Kiswahili. Waliambatana pia na wafanyabiashara kama vile Waarabu na baadaye Wahindi ambao walikuja kufanya biashara zao. Hawa wote walikuwa wakitumia lugha ya Kiswahili, na wengine kueneza dini ya Kiislamu

Katika sura hii tutaona pia kuja kwa Wabelgiji ambao walifika wakiongea Kingwana, lahaja ya Kiswahili ambayo hutumika nchini Kongo.

## 2.1 HISTORIA FUPI YA LUGHA YA KISWAHILI NCHINI RWANDA

Lugha ya Kiswahili iliingizwa nchini Rwanda na Wajerumaini, Wakoloni wa kwanza katika Afrika Mashariki na Kati. Koloni za Wajerumani zilikuwa Tanganyika (Tanzania ya sasa) Rwanda, na Urundi (Burundi ya wakati huu).

Wazungu hawa walikuja Afrika ya Mashariki na ya Katika karne ya 19. Tofauti na wakoloni wengine kama vile Wafaransa na Waingereza ambao walitawala na kueneza utamaduni wao na lugha zao. Wajerumani hawakufanya hivyo. Wakoloni hawa walitawala kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Chimerah katika mswada wake anasema: Wazungu hawa hawakutaka kuingiliana kitamaduni na wenyeji wa makoloni yao sababu waliaudharau kabisa utamaduni wa Waafrika, ukiwa ni pamoja na ule wa Waswahili. Hivyo hawakutaka Waafrika, kwa mfano, wajifuunze lugha yao tukufu ya Kijerumani. Kwa bahati Kiswahili kikawa kimeenezwa sehemu kubwa ya Tanganyika na wafanya biashara wa Kiswahili na vile vile Waarabu waliozungumza Kiswahili. Wajerumani wakaichukua lugha hiyo na kuifanya chombo cha mawasiliano baina yao na Waafrika badala ya kuwafundisha watawaliwa Kijerumani. Kwa njia hii, Kiswahili kakaenea katika nchi zote zilezotawaliwa na Wazungu hawa. Wakati wajerumani walipopokonywa makoloni haya baada ya vita vikuu vya kwanza vya ulimwengu, Kiswahili kilikuwa chasemwa na idadi kubwa ya watu katika nchi za Tanganyika, Rwanda na Burundi".

Hata hivyo Wajerumani hawakuleta lugha ya Kiswahili peke yao, bali walifuatana na wamishenari ambao walikuwa wakitafuta wafuasi wao wa dini ya Kikristo. Wageni wengine walifuatana na watawala wapya hawa. Walikuwa Waarabu, waliokuwa wakitafuta wafuasi wa dini ya Kiislamu.

Wamishenari wa Kizungu pamoja na Waarabu walihakikisha kuutetea utawala wa Kijerumani kwa sababu wakoloni waliwapatia usalama wa kutenda lolote bila wasi wasi nchini Rwanda.

Kufuatana na historia, Kiswahili kiliingia Rwanda kuanzia 11 Disemba 1892. Wakati huu ndipo nchi ya Rwanda ilipoanza kupokea wageni wa kwanza waliotumia lugha ya Kiswahili.

Tunaambiwa na Ntawigira (1997) kwamba Kiswahili kiliingia nchini Rwanda kwa kupitia sehemu nne muhimu za nchi; "sehemu ya kwanza ni ile iliyopitiwa na Mjerumani Dkt Oscar Bauman na watu wake. Alifika nchini Rwanda 1892 na alikuwa na watu wengi wakiwemo wanajeshi pamoja na wapagazi. Aliingia nchini Rwanda kwa kuvuka mto wa Akanyaru ulio kusini mwa Rwanda. Ni wazi kwamba hawa woate waliingia Rwanda wakiongea lugha ya Kiswahili kwa kujaribu kuwasiliana na Wanyarwanda, kwa lugha hiyo.

Ntawigira anasema pia kwamba sehemu ya pili ni kuingia kwa VON GOTZEN aliyevuka mto wa Kagera, kupitia mashariki mwa Rwanda mwaka 1894.

Alifuatana na watu 362. Jinsi Wajerumani hao walivyosonga mbele kwa kutaka kuonana na viongozi wenyeji wa Rwanda, ndivyo Kiswhaili kilivyojipenyeza katika jamii ya Wanyarwanda.

Sehemu ya tatu na ya nne ni kupitia magharibi na kaskazini magharibi mwa Rwanda, ambapo Wabelgiji walipitia kutoka koloni yao ya awali, iliyokuwa ikiitwa "Congo Belge" au Kongo ya Kibelgiji. Hawa walikuwa wakiongea Kingwana au Kiswahii cha w Kongo. Baadaye kidogo, Wabelgiji wengine walipitia Gisenyi wakitokezea mji wa Goma ulioko Kongo, kwenye mpaka wake na Rwanda, upande wa kaskazini magharibi. Wazungu hawa kutoka Kongo walikuwa wakizungumza Kiswahili pamoja na askari wao.

## 2.2 LUGHA YA KISWAHILI WAKATI WA UTAWALA WA WAJERUMANI

Hii ilikuwa kati ya mwaka 1898-1916 watawala hawa walitumia Kiswahili kama lugha ya mamasiliano kati yao na pia lugha ya kuunganisha maeneo yao yote ya utawala.

Kwa hali hii Chiraghdin na Mnyampala ( 1977:68) wamesema;

"kadhalika, kuanzia mwaka 1888, Majerumani walipozihodhi sehemu hizo za mrima na bara lake walikitumia chombo chicho hicho Kiswahili kutawalia. Wakatawala kwa kutumia maakida na majumbe na hawa wote wakatarajiwa na

utawala wa kijerumani kutumia Kiswahili. Wajerumani wana sifa ya kuwa wafanyapo jambo hujaribu kulifanya timamu kweli kweli basi kwa upande wa Kiswahili walianza uchunguzi wa lugha na desturi za waswahili na mapema, na maofisa wao wakawa wafunzwa lugha ya Kiswahili barabara kabla ya kuletwa katika koloni yao"

Hali kama hii iliwafanya Wajerumani kuanzisha shule za kufundisha Kiswahili Wanyarwanda ili waongeze idadi ya wazugumzaji wa lugha ya Kiswahilii kwa maana ya kuzidisha idadi ya wafanyakazi kwa kuwasiliana bila shida.

Mnamo mwaka 1901, kulianzishwa shule ya kwanza huko Nyanza, karibuna makao makuu ya Mfalme wa nchi ya Rwanda. Yasemekana kwamba mwanzilishi wa shule hiyo ya watoto wa viongozi, alikuwa amepachikwa kwa jina, Bwanakweli, mzungu ambaye alianzisha shule za kuandaa vijana wa Kinyarwanda kuwa viongozi wa baadaye. Mpango huu wa Wajerumani kusambaza Kiswahili kote nchini Rwanda uliendelea kwa kusaidiwa na wakalimani wa Kijerumani ambao wengi wao walikuwa ni watanzania. Pia wanafunzi walikuwa wanamaliza mwaka mmoja au miwili shuleni wakifundishwa lugha ya Kiswahili na uongozi, ile wasaidie wakoloni katika kutawala wao.

Mnamo mwaka wa 1912 Wajerumani waling'amua kwamba walishadanganyika kwa vile waliendeleza lugha ya Wafrika ilhali wakoloni wenzao Waingereza na

Wafaransa walikuwa wakifundisha lugha zao kwa kueneza ubwana na ufahari wao kupitia lugha zao na utamaduni wao.
Hivyo walianza kubadilisha na kupanda upya sera za lugha mashuleni ziwe ni kufundishia lugha ya Kijerumani na kutupilia mbali Kiswahili.

Haya yalikuwa mawazo kutoka kwa makasisi Wazungu (White Feathers) kutoka Tabora, nchini Tanzania kutoendelea na makosa waliyoyafanya Tanzania kwa kufundisha wakristo Kiswahili lugha ambayo ilikuwa inafungamana na dini ya Waislamu.

Kwa bahati mbaya mpango huu wa Wajerumani hawakufikia lengo kwani mwaka 1914 walipiga vita vikuu vya kwanza na kuletea ushindi Wabelgiji ambao walikuwa wakoloni wa nchi ya Kongo.

Kama inavyojulikana vita hivi jinsi vilipiganwa ulaya nzima vile vile vilisambaa Afrika nzima. Maana huko Afrika mashariki vita vilikuwa baina ya Waingereza na wajerumani na kupelekea ushindi wa Waingereza. Na baadaye kuichukua Tanganyika na kuitawala pamoja na Kenya na Uganda.

Wabelgiji walipofika hawakupata shida ya kuwasiliana na wenyeji wa Rwanda kwa vile walikuwa wakiongea Kiswahili walichofundishwa na Wajerumani. Vilevile Wabelgiji walikuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili lakini

Kiungwana ambacho tofauti yake na Kiswahili sanifu ni Kidogo kiasi cha kuwezesha watu kuwasiliana. Hebu tuone maoni kuhusu Kingwana, Ireri. (1991)

"Ingawaje, kamati ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki, iliweza kuwajulisha watawala wa Kongo ya Ubelgiji kwamba tofauti kati ya Kingwana na Kiswahili sanifu ilikuwa ni matamshi yasiyofuata kanuni za sarufi. Maoni hayo ya kamati yalipelekwa kwa watawala wa Kongo na Bwana Sandrart wa kutoka Rwanda alliyetumwa na Kongo ya Ubelgiji kuhudhuria mkutano wa kumi na tatu(13) wa kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki mnamo 1950. Bwana Sandrart aliweza kufahamisha kamati mambo kadhaa kuhusu Kingwana. Tofauti za kimatamshi hazikutatiza kueleweka kwa Kiswahili katika kukisanifisha ndiko kulikopendekezwa na Roehl katika Zaire, Rwanda na Burundi."

Baada ya muda mfupi Wabelgiji waling'amua kuwa Kiswahili kilikuwa na athari za utawala wa Kijerumani na kuanza kutenga lugha hiyo na kukuza lugha ya Kifaransa badala yake.

Lugha ya Kiswahili ilisitishwa kutumika mashuleni na hata kwenye kazi na ofisini. Mwaka wa 1929 ndiyo kumethibitishwa rasmi usitishaji wa matumizi ya Kiswahili mashuleni na mkaguzi wa ufundishaji wa kikoloni kutoka serikali kuu ya koloni za Wabelgiji huko Kongo Leopoldville(leo ni Congo Kinshasa). Tangu wakati huu Kifaransa kilitumiwa rasmi katika nyanja zote za utawala, na kufundishia shule zote tangu shule za msingi hadi vyuo vikuu mpaka leo hii.

Ijapo Kiswahili kimefutwa mashuleni pamoja na mambo ya kiserikali, lugha hii imeendelea kuemea na kusambazwa na wafanya biashara ambao hutoka Afrika ya Mashariki na pia wale wanaokaa na majirani wao kwa upande wa Kongo Magharibi mwa nchi ya Rwanda.

## 2.3 KISWAHILI NCHINI RWANDA BAADA YA UHURU

Kuhusu matumzi ya lugha baada ya uhuru Kifaransa kiliendelea kuwa lugha ya fahari na kutawala lugha nyingine ambazo zilikuwa zikitumika nchini Rwanda kama vile Kinyarwanda na Kiswahili. Wananchi wa tabaka zote walikiona Kifaransa kama lugha ya ustarabu na walitumia lugha hii katika nyanja zote kwa mfano katika utawala, shuleni na kibiashara Kifaransa kilitumiwa kwa mapana.

Hata hivyo sehemu ya biashara kwa vile wananchi hufanya biashara zao za nje na ndani pamoja na watu ambao huzungumza Kiswahili… Ndiyo sababu kubwa ya wazungumzao lugha hii. Kabiligi Augustin (1987) anasema; "Mnamo mwaka 1977 Rwanda na Tanzania ziliamua kushirikiana katika Maswala kadhaa na baadhi ya hayo ni ufundishaji wa Kiswahili sanifu katika ushirikiano wa elimu na utamaduni. Baada ya 1979 walimu wengi wameendelea kuletwa nchini hadi Rwanda kutoka Tanzania Rwanda hufundisha Kiswahili katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Pia idhaa ya Redio Rwanda hupeperushwa hewani nchini Rwanda"

## 2.4 KISWAHILI NCHINI RWANDA BADA YA MAUAJI YA 1994

Wakati huu Rwanda palikuwa na maisha magumu kwani kila kitu kiliharibika: Watu wengi walifariki, mali ziliibiwa, nyumba, mimea, mifugo vyote viliharibika. Lakini kuhusu lugha ya Kiswahili na wazungumzaji wake waliongezeka. Sababu kubwa ni wakimbizi wa zamani wa mwaka 1959 pamoja na wale wakaribuni wa mwaka 1994. hawa wote walirudi wakiangaa vizuri Kiswahili haswa wale waliokuwa wamekimbilia nchi za Tanzania, Kenya, Kongo na hata nchini Burundi. Hawa wote wengi wao walitumia lugha ya Kiswahili kama ndiyo lugha mama, sana sana watoto na vijana.

Idadi kubwa ya watu popote nchini iliweza kuongea Kiswahili kiasi kwamba tangu mwaka 1996 shule nyingi za msingi kwenye mikoa inayopakana na Tanzania ilikuwa ikifunza lugha ya Kiswahili baadaye kutahiniwa kwa lugha hiyo ili watoto wachaguliwe kwenda shule za sekondari.

Sera hii ilipewa mpango wa miaka mitatu kwa wanafunzi wa shule za msingi na walianza kujifunza Kinyarwanda ambacho ndiyo lugha pekee ya wenyeji na pia ya mawasiliano nchini.

## 2.5 HITIMISHO

Katika sura hii tumeona historia fupi ya kuenea kwa lugha ya Kiswahili na kufika mpaka Rwanda miaka mia moja iliyopita. Tuligusia pia wakoloni wa Kijerumani ambao ndio wameleta Kiswahili nchini Rwanda wakoloni hawa walitumia lugha hii waliyoikuta Tanganyika, nchi mojawapo ya Afrika Mashariki ambayo

wenyeji wake walikuwa wazungumzaji wa lugha hii iliyosambazwa na pia pwani za nchi ya Kenya.

Lugha ya Kiswahili imetumiwa kama chombo cha mawasiliano baina ya watawala wa Kijerumani na watawaliwa wa mataifa ya Tanganyika Rwanda na Burundi kama tutakavyoona katika sura nyingine hapo baadaye.

Katika sura hii tuliona pia jinsi wanadini walivyoitumia lugha hii kwa kuhubiria dini zao na kutafuta wafuasi kama vile dini ya Kikristo na hasa dini ya Kiislamu.

Tuliweza kunukuru pia wandishi sehemu nyingine ambao wametoa maoni yao kuhusu lugha ya Kiswahili ilivyo kabiliana na mazingira magumu, katika shule mbalimbali kutoka nchi tofauti hususan zile za Afrika ya Mashariki.

Na mwisho tuliona jinsi lugha ya Kiswahili ilivyofifia shuleni, ofisini wakati wa utawala wa Kibelgiji na badala yake kukakuzwa lugha ya Kifaransa, lugha ambayo ilikuwa mojawapo ya watawala wa wakoloni hao.

Vilevile tuliona jinsi lugha hii ilivyotumiwa shuleni baada ya uhuru lakini kwa kiasi kidogo. Ufundishaji wa somo la Kiswahili unaeendelea kupanuka siku hadi siku katika nchi mbalimbali n.k. nchi ya Rwanda ikiwemo. Hali hii inasababisha haja ya kujua na kufanya utafiti mbalimbali katika elimu za sekondari, vyuo vya walimu pamoja na vyuo vikuu.

## 2.6 AFRIKA YA MASHARIKI NA YA KATI

Katika sehemu hii nitazungumzia lugha ya Kiswahili katika mataifa jirani ya nchi ya Rwanda.Bila shaka ni nchi za kaida hii ya Maziwa makuu ambazo zimeizunguka Rwanda na kuwasiliana kwa njia mbali mbali, ikitumia hasa lugha ya Kiswahili.

Nchi hizi ni pamoja na Tanzania inayopatikana mashariki mwa Rwanda, nchi ya Burundi iliyoko kusini mwa nchi ya Rwanda, Kongo inayopatikana magharibi mwa Rwanda, na Uganda, iliyopo kaskazini, kisha nchi ya Kenya ambayo hata ijapokuwa haipakani na nchi ya Rwanda moja kwa umoja, hii hali kadhalika ni nchi muhimu kwa Rwanda, sana sana kwa upande wa mawasiliano ya kibiashara , ambayo ni uti wa mgongo wa kila nchi. Kumbuka kwamba nchi ya Rwanda haina mkondo wa bahari ambapo inaweza kutumiwa kupeleka na kupokea bidhaa zake kutoka ng'ambo. Kwa hivyo,njia kuu ya kusafirisha bidhaa ni aidha kivuko cha Dar es Salaam, Tanzania au Mombasa, Kenya.

Katika sura hii tutaona vile vile jinsi ambavyo kila nchi inachangia kwa kuendeleza lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Rwanda. Vilevile tutaweza kumulika matatizo na athari za kila nchi baina ya hizo zilizotajwa hapo juu, na aidha ukuzaji wa Kiswahii katika elimu nchini Rwanda.

Kama tulivyosema hapo awali, Kiswahili ni lugha muhimu katika nchi ya Rwanda na vile vile hali ilivyo Afrika Mashariki na ulimwengu mzima. Haya yanapata ushahidi katika madai ya Chiraghdin (1977:67) "Kiswahili leo kimekuwa kama

mto uliotanda katika eneo kubwa kuliko eneo lake la asili, na ni lugha mojawapo kati ya lugha nne ambazo zimeenea Afrika; hizo lugha nyingine ni Kiarabu, Kifaransa na Kiingereza. Kati ya hizo, Kiswahili peke yake ndiyo lugha yenye asili ya Kiafrika iliyoenea sehemu kubwa ya Afrika na hata ikavuka mipaka ya Bara Afrika. Kwa hivyo, kama ilivyotangulia kutajwa, Kiswahili ni lugha pekee katika Afrika iliyoweza kuwaathiri Kiafrika-lugha na utamaduni wa watu wasiokuwa Waafrika. Kwa sababu ya umuhimu wake, hakuna lugha nyingine ya Kiafrika iliyoikaribia hadhi ya Kiswahili kwa kutangazwa zaidi katika idhaa za dunia au kusomeshwa zaidi katika vyuo vikuu katika nchi mbalimbali.

## 2.7 HISTORIA FUPI YA KISWAHILI NCHINI KONGO

Mnamo mwaka 1850, Sultani wa Unguja aliweza kuimarisha utawala wake katika pwani ya Afrika Mashariki. Tangu wakati huo biashara ilianza kupanuka na kuenea bara mpaka huko Kongo. Misafara ya Tiputip, kwa mfano, ilikuwa na watu zaidi ya 4000. Walikuwa wakizungumza Kiswahili-Walikaa miezi kadhaaa na pengine zaidi ya mwaka wakitafuta watumwa na pembe za ndovu.

Chiraghdin na Mnyampala (1997) wameandika kwamba wakati misafara hii ilivyokuwa ikizidi kwenda magharibi ikawa inaimirisha vyengo vyao, na mpaka leo miji ya Zaire (ambayo sasa ni jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo) ina majina ya miji ya Pwani Afrika Mashariki. Kwa mfano, Kongo kuna sehemu inayoitwa "Tongoni" na ambako unatumika Kiswahili; na jina hili Tongoni ni la kitongoji kilichoko upande wa Kaskazini mwa Tanga. Pia wanaendelea kuandika;

> "Watu hao wa Mrima wakaimarisha biashara na lugha yao ikaenea. Wenyeji wakawa wawaita Wa(u) ngwana na lugha yao ya Kiswahili ikawa Ki(u) ngwana. Lakini hapo tena kile Kiswahili kilikuwa pia kimechukua maneno na matamshi ya lugha za Kimanyema na pia Kibelgiji (Kifaransa), lugha ya watawala wa wakati huo". P. 84

Wabelgiji walikitumia Kiswahili katika kuimarisha utawala wao. Kwa mfano, waliajiri askari wakitumia lugha ya Kiswahili hasa sehemu za mashariki; kusini na kaskazini mwa nchi ya Kongo. Askari wa sehemu za kati na Magharibi mwa nchi hiyo ya Kongo walitumia lugha ya Lingala. Vilevile Ksiwahili kilizidi-kuenea kwa sababu ya maingiliano ya wafanyakazi katika machimbo ya migodi ya shaba huko Katanga. Pia lugha ya Kiswahili ilitumika katika mipaka ya Tanzania na Congo, Zambia, Rwanda na Burundi.

Wamisheni nao pia walikitumia kwa kufundishia dini katika shughuli zao, na wakatoa vitabu na magazeti na pia kufundishia shuleni. Hata hivyo, serikali ya Kibelgiji ilipendelea kukieneza Kifaransa na hivyo basi ikawa inapinga lugha ya Kiswahili, hasa kati ya mwaka 1930 na 1940.

Kinyume cha serikali ya Wakoloni na misheni, chama cha Walowezi kwenye machimbo ya migodi huko Katanga, kilihimiza Waafrika kutumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kati yao. Kwa sababu hii wapigania uhuru wa chama cha

"confideration of Katanguaise Association", chini ya mwenyekiti Moise Tchombe, walitumia Kiswhaili. Makala ya walowezi wa Kibelgiji pia yalitumia lugha tatu, Kifaransa, Kiflemishi na Kiswahili

Pia, wanachama cha ushirika wa Katanga au "union Miniere dekatanga" walikuwa na gazeti liitwalo"Mwanachama," mwaka 1960. Gazeti hili liliandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Hivi leo nchini Congo kuna lugha zipatazo 200. Kati ya hizi lugha zinazotumiwa ni Kiswahili Kilingala, Kiluba na Kikongo. Hata hivyo kuna tofauti ya matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, kuna tofauti baina ya Kiswahili kisemwacho Katanga na kisemwacho Kisangani. Lakini kunafanywa juhudi za kutumia "Kiswahili Sanifu" ili kupatikana mawasiliano na nchi za jirani zinazotumia Kiswahili.(Chimerah 2000)

## 2.8 KISWAHILI NCHINI BURUNDI

Misafara kutoka Ungunja kupitia Tabora mpaka Ujiji, kuelekea nchini Kongo ilipitia nchini Burundi. Hivyo basi watu wengi hawakuwa wanafika wote Kongo, bali wengine walikuwa wakibakia njiani kwa ajili ya kuchoka au maradhi. Inaonekana kwamba misafara hiyo iliathiri vituo muhimu vitatu, ambavyo ni Tabora, Ujiji na Buyenzi (Kitongoji cha Waislamu mjini Bujumbura, Burundi).

lonekanavyo, hii ndiyo sababu siku hizi watu wa Bujumbura, kama wale wa Manyema, hudai kuwa Kiswahili Chimbuko lake ni Burundi au Congo

Nchini Burundi, Kiswahili husomeshwa kama somo la lazima katika vituo na vyuo kadhaa vilivyoko katika mji mkuu wa Bujumbura, na karibu na mji huo mkuu. Vituo hivyo ni kama vile Taasis ya mafunzo ya Kijeshi (Institute Supereur des Cadres Militaires). Bigirumwami (1983) anaseema kwamba, pamoja na Taasis za uhasibu na mawasiliano, kufikia mwaka 1983 kulikuwa na mipango ya kuanzisha masomo ya Kiswahili katika Taasisi ya Elimu ya uandishi wa habari.

Burundi pia ina mpango na Tanzania ambao unaiwezesha kupata walimu wa Kiswahili kutoka nchi hiyo jirani. Kwa sasa walimu hao wanasomesha Kiswahili nchini Burundi. Kuhusu utangazaji, Kiswahili kinatangazwa asili mia 35 ya muda wote wa matangazo idhaa ya nje ya Burundi. Muda uliyo baki, asilimia 65 hutumiwa kwa kutoa matangazo kwa lugha ya Kifaransa. (Bigirumwami 1983)

## 2.9 KISWAHILI NCHINI TANZANIA

Hapa tunatazama Kiswahili kwa awamu tatu; nazo ni:

i) Kiswahili kabla ya wakoloni

ii) Kiswahili wakati wa wakoloni, na

iii) Kiswahili wakati wa uhuru.

i) **Kiswahili kabla ya wakoloni**, hapa tuanzie Unguja ambako tumeona kwamba Kiunguja kilivuka ziwa na kufika Mrima.

Wakati wa enzi ya Sayyid Said, mji wa Unguja ulikuwa na mafanikio makubwa. Biashara nyingi zilivuma; wageni wa pwani na wengine kutoka bara wakaenea Unguja. Muda si muda wageni wa Kizungu kutoka sehemu nyingi za ulaya wakafika pia. Misafara ilianza kutoka Unguja na kushukia kwenye kituo kikubwa cha Bagamoyo. Misafara hiyo imeuendelea na kuingia bara ndani. Lugha iliyokuwa ikitumiwa ilikuwa ni Kiswahili.

Wazungu walifika Unguja walikuja kwa sababu mbalimbali. Baadhi yao walikuja kwa sababu za kibiashara wengine walikuja kwa lengo la kueneza dini ya Kikristo; na wengine walikuja kwa minajili ya kutalii.

Wakati huo wamishenari kama vile Bishop Steere, walikiona Kiswahili kama lugha inayofaa kwa kufundisha dini na kueneza Ukristo; barani Afrika, maana walipotangamana na wenyeji waliweza kuwasiliana nao kwa urahisi wakitumia lugha ya Kiswahili.

Wamisheni hawa kwanza waliitalii lugha ya Kiswahili mpaka wakaanza kuandika sarufi yake. Hapo ndipo wakaifasiri injili na kuwahubiria wafuasi wao.

**Kiswahili wakati wa wakoloni**

Wakoloni wa kwanza kuja Tanganyika walikuwa Wajerumani. Watawala hawa walipofika mwaka 1888 walitumia Kiswahili kama chombo cha kutawalia. Kama kawaida wakoloni hutumia wenyeji kwa kunyanyasa wenyeji nduguzao. Ni wakati huo huo Wajerumani walipotumia maakida na majumbe kwa utawala wao. Hawa wote walikuwa wakitumia lugha ya Kiswahili.

Utawala wa Kijerumani ulitayarisha majeshi na maofisa wengine wakitumia Kiswahili. Mwisho wakulima, wafanyabiashara na wamisheni walitoka Ujerumani tayari wakizungumza lugha ya Kiswahili. Walipofika Tanganyika walianza kujenga shule na kwanza kufundisha vijana wenyeji kwa lugha ya Kiswahili.

Japo wamishenari wengine walipendelea kufunzwa kwa lugha za kienyeji za Uafrika, wakidai kwamba wafuasi na wanafunzi wataelewa zaidi wakihubiliwa kwa lugha ya kabila lake. Hata hivyo nchini Tanzania lugha ya kufundishia imeendelea kuwa ya Kiswahili wakati wa utawala wa Wajerumani sana sana kwa kupitia wamishenari wa U.M.C.A. Hawa walijenga shule zao, wakatoa vitabu na kuwa wa kwanza kutoa magazeti ya Kiswahili.

Waingereza kutawala Tanganyika; baada ya watawala hawa wapya kuwashinda Wajerumani katika vita vya pili 1914 – 18 wakaanzisha utawala nchini humo.

Waigereza pia waliona kwamba mpango huu wa kujenga utawala wa wakoloni ni mzuri kwa kutumia Kiswahili.

Hata hivyo baada ya muda si mwingi Waingereza waliona kwamba watakabiliwa na shida iwapo wataendelea kufundishia Kiswahili peke yake. Ndipo Waingereza wameanzisha mpango mpya wa masomo. Walianza kuigawa sehemu tatu za kuweza kugawa lugha za aina tatu. Shule za mwanzo zilifundishwa kwa lugha za makabila mbali mbali ya Watanzania. Shule za kati zilifundishwa kwa kutumia Kiswahili. Na shule za juu zilitumia lugha ya Kiingereza kwa mafunzo lakini hata hivyo utawala uliendelea kutumia Kiswahili na raia huko makwao. Tuseme kwamba Kiswahili kilibaki kuwa lugha ya raia ambao hawakuenda shule. Wakati mwengine Kiingereza kikawa lugha ya juu au ya watu waliokwenda shule.

Pamoja na hayo, isipokuwa sehemu fulani fulani, Kiswahili kimeendelea kuwa lugha ya Watanzania walio wengi. Kiswahili kilitumiwa kwa magazeti kadhaa. Vyama vya wenyeji wa Tanganyika vilitumia Kiswahili. Chiraghdin (Idem) anaandika;..."kwa mfano, chama cha wafanyikazi wa serikali. (Tanyanyika Territory Civil Servants Association), Kilichobuniwa Tanga 1922, kilikuwa na gazeti lake lililoitwa "kwetu" na lililotoka baina ya 1937 na 1952. Chama cha siasa kilichokitangulia TANU yaani Tanganyika African Association (TAA) kilikuwa na katiba yake ilioyandikwa kwa Kiswahili.

Vilevile chama cha TANU kilipobuniwa mwaka katika juhudi zake za ukombozi. Na mwaka 1955 Kiswahili kikaanza kutumiwa bungeni, na ilipofika 1960 Chama cha TANU kikaanzisha azimio la kukifanya Kiswahili lugha ya taifa". Tokea hapo juhudi zilifanywa ili Kiswahili kitumike katika shughuli za serikali.

**(iii) Kiswahili wakati wa uhuru**

Chama cha TANU kilipoazimia kuwa Kiswahili kiwe lugha ya taifa hapakuwako na wasiwasi wa kufikiria lugha nyingine ya kienyeji kufika chukua hiyo.

Rocha Chimerah (2001) anasema!

"Wanasiasa Waafrika huko Tanganyika, chini ya Raisi Mwalimu Nyerere, baada ya kuchukua uongozi wa nchi, hawakupoteza wakati bali walipitisha kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa ya nchi yao. Tanganyika ilipoungana na kitovu cha Uswahili eneo hilo, Zanzibar, mnamo mwaka wa 1964, mambo yakazidi kuoga. Muungano huo ulikipa Kiswahili nguvu zaidi. Kiasi cha kwamba Azimio la Arusha la 1967 likahakikisha ya kuwa Kiswahili sio lugha ya Taifa ya Tanzania tu, bali pia ndiyo lugha rasmi, wala sio Kiingereza. Kwa sababu hii, Kiswhaili kikapatiwa nafasi kubwa sanaa katika nyanja zote za maendeleo ya Kitaifa kama vile utawala, elimu na nyinginezo."

Ni kweli kwamba baada ya kupata uhuru, nchi ya Tanzania ilikuza Kiswahili kwa haraka na kwa ustadi mkubwa.

Kwa mfano katika mwaka 1964 kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iligeuzwa kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Taasisi inashirikiana sana na idara na Taasisi zingine za ukuzaji wa Kiswahili ambazo ni idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salam; Taasisi ya Elimu ya Taifa; sehemu ya Kiswahili ya wizara ya maendeleo ya jamii, utamaduni, vijana na michezo; UKUTA- shirika la watu binafsi la kukuza lugha na hasa ushairi nchini Tanzania; NA BaKITa – Baraza la Kiswahili la Tanzania; na mashirika mengine ya kukuza lugha ya Kiswahili.

## 2.10 KISWAHILI NCHINI KENYA

Jinsi misafara ilivyokuwa huko Unguja kuelekea Mrima na kwenda bara la Tanganyika ndiyo vile ilivyokuwa upwa wa Kenya kwenda bara yake. Lakini inajulikana kwamba misafara iliyokuwa ikianza Mombasa na Malindi ilikuwa si kwa wingi kama ile iliyokuwa ikianzia Unguja.

Sababu kubwa ya tofauti hizo ni kwa sababu ya wakoloni wao. Tanganyika imetawaliwa na Wajerumani ambao wameipokea lugha ya Kiswahili kwa mikoni miwili. Wakati huo kwa upande wa Kenya, wenyeji wao walipigana na Muingereza wakati alipoingia. Vita vimesita mwaka 1895, kwa sababu hii wenyeji wa upwa na miji yao hawa kustawisha biashara kama ilivyokuwa Unguja.

Hata hivyo, kulikuwako na misafara ya biashara iliyokwenda bara ikiwasiliana na wenyeji kwa lugha ya Kiswahili. Wazungu walioingia bara walifuata nyayo za misafara ya Waswahili waliyotoka upwa wa Kenya. Kama ilivyokuwa kwa bara la Tanzania ndivyo ilivyokuwa kwa bara la Kenya kabala ya kuja kwa wazungu. Lakini kwa upande wa Kenya Waingereza walianza kukididimiza Kiswahili. Misheni ya Kiingereza vilevile hawakupendelea Kiswahili, kwa sababu walidai eti Kiswahili kimefungamana na Uislamu. Wamisheni hawa walipendelea kufunza kwa lugha za kikabila kwamba ilikuwa rahisi kuwafundisha watoto kwa lugha yao wenyewe.

Tuone mswada wa Rocha Chimerah (2001)

"...kwa ujumla, Kenya haikukiuka sana hatua zilipopigwa na Tanzania katika hali ya kukiendeleza Kiswahili, japo katika nchi hii, kilikuwa na upinzani, sana sana kwa sabbu ya mfumo wa "...siasa ya kikoloni, iliyopendekeza Kiingereza zaidi dhidi ya lugha za Kiafrika. Katika nchi hii, badhi kubwa ya wale waliochukuwa mamlaka kutoka kwa Waingereza walipendelea Kiingereza na mambo ya Kizungunzungu. Hawakuona ni jinsi gani Kiswahili kinavyoweza kuwaendeleza kibınafsi na vilevile kitaifa..."

Kiswahili kiliendelea kupigwa vita na serikali ya wakoloni. K.M. mnamo mwaka Sir Charles Eliot aliyekuwa Gavana wa Kenya alihimiza lugha za makabila

mengine na kuifanya Kenya iwe chini ya wazungu na kusiwe na kiungo chochote cha lugha ya Kiafrika. Hali hii ya kukipiga vita Kiswahili iliendelea sana, na mnamo 1935 Kiingereza kikawa ndiyo lugha ya mtihani katika shule ya msingi, na mwaka huo kukawepo na tume ya Kifalme ya Afrika ya Mashariki ya kutoa ushauri wa matumizi ya lugha shuleni. Hata hivyo wanasiasa walijaribu sana kukitilia mkazo Kiswahili yangu awali, na polepole kikaanza kuwaungunisha wananchi katika harakati za ukombozi. Kwa mfano, Rais wa kwanza wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta amehimiza matumizi ya lugha ya Kiswhaili. Baadaye (1974) serikali ilipitisha azimio Kirasmi kwamba, Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa ya nchi ya Kenya.

Kuhusu maendeleo ya lugha ya Kiswahili wakati wa utawala wa Daniel Arap Moi, aliyechukuwa uongozi baada ya Kenyatta kuangdumia Rocha Chimerah (200:100) anasema:

"…hatua iliyopatikana ni kwamba Kiswahili, kuanzia mwaka wa 1984, kilifundishwa katika shule zote, kuanzia msingi hadi upili. Si hivyo tu, bali sasa Kiswahili ni somo la lazima sababu, kama somo sawa na Kiingereza na Sayansi. Njia hii ya kulipatia umuhimu somo, ndiyo njia bora zaidi ya kukifanya Kiswahili kistaiwe na kuthaminiwa Kitaifa. Ni muhimu pia ibainishwe ya kwamba Kiswahili ni somo la kikati kabisa katika "zutafindaki" (vyuo vikuu) zote za Kitaifa nchini."

## 2.11 KISWAHILI NCHINI UGANDA

Kiswahili ni lugha ya kwanza ngeni kutumika Uganda kabla ata Mzungu wa kwanza kufika pande hizo mwaka 1862. Kabla ya hapo Waswahili walikuwa wameshakieneza Kiswahili katika shughuli za biashara, dini n.k.

Wazungu walipoingia Uganda walikikuta Kiswahili kikitumika kama vile walivyokikuta kikitumika nchini Tanzania na Kenya japo huzidiana kwa kiwango fulani. Wazungu hawa kuona hivyo, walianza kueneza mambo yao ya Kiserikali na dini ya Kikristo. Chiraghdin na Mnyampala (1977) wanasema: Wanavyoandika"...mwezi Novemba 1878, Bishop Mackay alisema kwamba kwa bahati nzuri Kiswahili kinafahamika sana, nami nakijua vizuri na nina vipande vingi vya agano la kale na Agano Jipya kwa Kiswahili. Basi mara nyingi hueza kumsomea neno la Mungu, Mfalme na baraza lake lote..."

Baada ya muda mfupi wamisheni walianza kukipinga Kiswahili na kusema kuwa kiliafungamashwa na Uislamu. Lakini wakati huo walikuwa wameshajifunza Kiluganda.

Lakini utawala wa serikali uliendelea kikipendelea Kiswahili katika shughuli zake. Chiraghdin na Mnyampala (Idem) wanaendelea kusema "katika hoja ambazo Gavana wa Uganda wakati huo, W.F. Gowers, alizipeleka kwa Waziri wa Makoloni katika mwaka 1927 alisema kuwa Kiswhaili kitumiwe Uganda kuwa ndiyo lugha ya kutumiwa na wote na ya kusomeshea tanigu shule za msingi ili

kufuata mpango wa Kenya na Tanganyika. Alisisitiza kuwa kitumiwe Kiswahili zaidi kuliko Kiganda na Kiingereza, lakini Waganda na misheni walilipinga jambo hili. Badala yake wao wakahimiza matumizi ya Kiganda..."

Tangu hapo siasa ya serikali ya Uganda ilikuwa ni kukididimiza Kiswahili. Kwani mwaka 1953 tume ya mfalme ya Afrika Mashariki ikakataza matumizi ya Kiswahili au hata Kiganda. Wakati wa harakati za uhuru, chama cha UPC kilichokuwa kikiongozwa na Milton Obote, kiliiona haja ya kutumiwa Kiswahili nchini. Kwa hivyo kilipitisha azimio kuwa Kiswahili kifundishwe shule. Walikuwa pia na pendekezo la kufanya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa, Uganda. Lakini serikali hiyo ya U.P.C. ilikuwa ikitawala pamoja na Chama cha Baganda, kilikuwa kinaitwa "Kabaka Yekka" Chama hiki hakikupenda Kiswahili kitumiwe badala ya Kiganda na kilipinga azimio hilo.

Kiswahili nchini Uganda kiliendelea kukandamizwa mpaka mwaka 1971, wakati mapinduzi ya serikali na Rais Idi Amin. Aliwatangazia wananchi wa Uganda kuwa lugha ya Taifa itakuwa Kiswahili. Mpaka sasa Kiswahili kinabadilisha sura ya zamani kama tunavyoambiwa na Rocha Chimeraha (Idem) "..Hali ilivyo sasa, mwisho mwa karne ya ishirini (20) ni kwamba Kiswahili kinaendelea kupiga hatua kidogo kidogo hata huko kusini mwa Uganda. Raisi wa sasa wa nchi hii, Yoweri Kaguta Museveni, asema Kiswahili vizuri sana. Kwa sababu hii na nyinginezo, hasa kwamba watu wa Afrika ya Mashariki wanaanza kukariibiana tena na kuwa na uhusiano mzuri kama zamani, maendeleo ya Kiswahili yanashika

kasi Uganda. Kwa mfano, imeshaamuliwa kwamba, hivi karibuni, kitakuwa somo mojawapo muhimu katika shule za nchi hiyo kama ilivyo Kenya na Tanzania. Hivi sasa. Kiswahili kinafundishwa huko chuo kikuu cha Makerere na pia katika chuo cha Kiislamu, Mbale…"

## 2.12 HITIMISHO

Katika sehemu hii ya utafiti kuhusu Kiswahili katika elimu nchini Rwanda, nilitoa mapendekezo yangu huku nikitilia maanani ufundishaji bora wa lugha ya Kiswahili. Sasa hivi lugha ya Kiswahili si maarufu katika Afrika Mashariki tu bali katika Afrika yote na ulimwengu mzima.

Tuone vile Rocha Chimerah (2001) anavyoandika kuhusu Kiswahili kama lugha ya Kimataifa.

"..Kiswahili sasa ni lugha ya Kimataifa. Jambo la kwanza, imebainishwa kwamba lugha hii inatumiwa kwa mawasiliano na watu wa mataifa kadha barani Afrika, na pia kwingineko. Mataifa hayo ni kwanza, yale ambayo ni kitovu cha lugha hii, Kenya, Tanzania na Comoro. Pili ni ya ambayo raia wake wengi wanazugumza Kiswahili kama lugha ya pili. Haya ni mataifa ambayo baadhi ya watu wake wanawasiliana kwa Kiswahili kama lugha ya pili au ya tatu. Mataifa haya ni kama vile Malawi, Zambia, Zimbambwe (asilimia ndogo), Somalia, Sudan (kusini), Msumbiji (Mozambique – kaskazini) na Oman (thuluthi moja: wahamiaji kutoka Zanzibar). Vilevile kuna baadhi ndogo ndogo za watu wanatumia Kiswahili kwa mawasiliano huko Yemen, Emirates na hata Saudi Arabia".
Kiswahili pia ni lugha mojawapo muhimu katika shule za msingi na sekondari na pia katika vyuo vikuu ulimweguni.

# SURA YA TATU

## 3.0 HALI YA KISWAHILI KATIKA MFUMO WA ELIMU, RWANDA

Yafuatayo ni majibu kuhusu sera ya ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimu nchini Rwanda. Kabla ya kujibu maswali haya tungependa kufafanua mfumo wa ufundishaji nchini Rwanda.

Shule za msingi husomeshwa kwa muda wa miaka sita. Shule za upili huchukua pia miaka sita, mahali ambapo vyuo vikuu husomeshwa kwa muda wa miaka minne. Kwa hivyo nikusema kwamba mfumo wa masomo nchini Rwanda, humchukua mtoto miaka kumi na sita kuhitimu; Yaani tangu darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu; Hii ina maana ya mfumo wa sita-sita-nne.

i) Kwa kujibu swala la kwanza la utafiti wetu; Kiswahili huanza kufunzwa kidato cha 4 nchini Rwanda, hadi Chuo Kikuu kwa wale wenye kuchagua kujifunza Kiswahili. Somo hufunzwa kufuatana na mchepuo fulani; kwa mfano mchepuo wa masomo ya sayansi, mchepuo wa masomo ya biashara na kadhalika. Sasa Kiswahili kipo kwenye kundi la lugha.

ii) Somo la Kiswahili hutengewa saa nne kwa wiki katika kidato cha nne; saa tano katika kidato cha tano na cha sita.

Masaa haya ni kidogo ukilinganisha na masomo mengine,kwa mfano somo la Kifaransa hutengewa saa saba kwa wiki kwa kila kidato ilhali Kiingereza nacho hupatiwa masaa saba katika kidato cha nne, saa mbili katika kidato cha tano na saa mbili katika kidato cha sita. Wakati Kinyarwanda kina saa nne katika kidato cha nne saa tatu katika kidato cha tano na saa nne katika kidato cha sita. Kwa habari kamilifu zaidi, tazama jedwali lifuatalo:

**Ratiba ya wiki ya masomo lugha**

| | Kidato cha 4 | Kidato cha 5 | Kidato cha 6 |
|---|---|---|---|
| Kiingereza | 7 | 2 | 2 |
| Kifaransa | 7 | 7 | 7 |
| Kiswahili | 4 | 5 | 5 |
| Kinyarwanda | 4 | 3 | 4 |

Jedwali (i) Kipindi ni saa moja

Ukitazama jedwali, utaona ya kwamba hakuna tofauti kubwa ya vipindi kwa kila lugha isipokuwa lugha ya Kifaransa ambayo ina saa 21 kwa wiki, Kingereza kina saa 11 kwa wiki, Kiswahili kina masaa 14 kwa wiki, na Kinyarwanda kina masaa 11 kwa wiki.

Lakini kumbuka kwamba baina ya lugha hizi zote Kifaranza na Kiingereza hufundishwa tangu darasa la tatu katika shule ya msingi. Kinyarwanda, kwa upande mwingine hufundishwa tangu darasa la kwanza katika shule ya msingi mahali ambapo lugha ya Kiswahili hufundishwa tangu kidato cha nne, shule za upili. Hii ina maana kwamba Kiswahili hakitiliwi maanani zaidi katika elimu nchini Rwanda ukilinganisha na lugha nyingine zilizo tajwa hapo juu.

Lugha ya Kiswahili, kihadhi, inakuwa ya nne shuleni, lakini kwa hali halisi ni lugha ya pili ikifuatia lugha ya Kinyarwanda, ambayo ni lugha ya taifa. Kiswahili ni lugha ambayo inaongewa na watu wengi ambao ni wasomi na wale ambao si wasomi.

Bakari (1979) anatambua kwamba nchi nyingi za Kiafrika zina tatizo la utambulisho, kupitia lugha ya taifa. Anaeleza kwamba nchi nyingi za Afrika bado zina lugha za kigeni ambazo zinatumika kama lugha za taifa. Kwa matazamo wake Bakari, lugha ya kigeni si mwafaka kuwa lugha ya taifa, kwa sababu, huwanyima wananchi wanaohusika nafasi ya kufikia taasisi zao. Hivyo basi, anapendekeza lugha za kiasili zitumike kama lugha za taifa katika nchi za Afrika. Anasisitiza kwamba lugha ya kiasili kuwa lugha ya taifa ni swali muhimu katika utambulisho wa taifa. Kwa sababu, kwake yeye, utambulisho ni utamaduni wa pamoja ambao hushirikisha jamii kupitia lugha asilia ya taifa. Mtazamo wa Bakari ni muhimu sana kwa utafiti kama huu.

## 3.1 Hali ya Kiswahili katika Elimu

i) Lugha nyingine zimejibiwa hapo juu; labda tukumbushe zaidi hizo ni Kinyarwanda, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili.

ii) Kuhusu saa tazama jedwali (i)

iii) Lugha ya Kiswahili inatahiniwa kiwango gani/kitaifa?

iv) Mtihani wanafunzi wanaopewa ni wastani.

Dosari za uendelezaji wa Kiswahili shuleni siyo mpya katika Afrika Mashariki na Kati. Kwa mfano Chiraghdin na Mnyampala (1997:77) wanaosema mambo yafuatayo kuhusu Kiswahili:

"Waziri wa Elimu alitangaza kuwa Kiswahili kitafanywa kuwa ni somo la lazima katika viwango vyote vya shule pamoja na vyuo vya walimu. waliotoa maoni kuwa Kiswahili kitakuwa ni somo la lazima katika shule za sekondari ikiwa twataka tuwe wamoja, wa taifa moja, katika wakati mchache. Mawasiliano katika lugha hii ni kiungo muhimu kwa sababu lugha za kikabila ni nyingi mno, na Kiingereza kinasemwa na kufahamiwa na (watu) wachache sana. Pamoja na kuwa matamshi kama haya yamepata kutolewa Kenya na watu wenye madaraka katika elimu, lakini Kiswahili kimefanyiwa juhudi ndogo kabisa ukilinganisha na juhudi zinazofanywa kukipeleka mbele Kiingereza. Inaelekea kana kwamba zile mbegu zilizopandwa na kupaliliwa wakati wa enzi ya ukoloni sasa zimechipukiza na kusitawi, hasa tokea uhuru kupatikana. Kwa mfano darasa la mwisho katika shule ya msingi lina vipindi 45 kila juma. Kati ya hivyo, viwili , tu ndivyo vya

Kiswahili, kumi ni vya Kiingereza na vingine vyote vilivovyobakia ni vya masomo ambayo yanafunzwa kwa Kiingereza. Juu ya hayo, ingawa Kiswahili kinakubaliwa na kutiwa katika jedwali la masomo, lakini kwa kuwa hakifanyiwi mtihani, kimekuwa hakishughulikiwi kama inavyopasa, hata katika hivyo vipindi viwili na wanafunzi wanashawishwa kwa kila njia watumie Kiingereza wakati wote..."

### 3.2 Kuhusu walimu wa Kiswahili

i) Kutaka kuelewa kuwa somo la Kiswahili lina walimu wa kutosha wanapatikana. Pia inategemea shule zenyewe ziko mahali gani. Sanasana wakaguzi wa somo la Kiswahili wamesema kuwa shule za mijini hupata walimu wa kutosha, wakati ambapo shule za mashambani walimu mara nyingi hukosekana. Na sababu kubwa ni kwamba walimu katika shule za mijini wanaweza kufundisha hapa na pale ili wajipatie pesa zaidi katika muda wao wa ziada.

ii) Kuhusu swala la ujuzi wa walimu pia wahusika walisema kwamba ilikuwa vigumu kupata walimu wenye ujuzi kwa vile wale waliokuwepo kabla ya vita vya mauwaji ya kuangamiza, wengi wao wamefariki na wengine walitoroka. Kwa hivyo wachache waliobaki hawawezi kutosheleza . Hivyo basi ilibidi kuwaajiri wale wenye ujuzi bora pamoja na wale wa kadiri ili kukidhi haja.

Kuhusu swala la kule ambako walimu walipata mafunzo Mhojiwa mmoja alisema "walimu tunawapata kutoka Tanzania, wale ambao walirudi nchini Rwanda baada ya vita vya 1994. Na wengine tunawapata kutoka nchini Kongo (nchi iliyokuwa Zaire ya zamani)."

Kumbuka kwamba hawa walimu kutoka Congo hawawezi kuongea kwa Kiswahili sanifu nyakati zote. Kiswahili sanifu (kwa maoni yangu hawa walimu wanajifunza Kiswahili wakati wanapofundisha watoto wa shule). Kupenda kujua iwapo wanapata semina na mafunzo mara kwa mara walimu ambao niliwahoji waliomba swala hili liwe kama pendekezo lao na kujibu kuwa hawapati mafunzo yoyote ya kuwawezesha ujuzi kutoka kwa walimu wenzao wa Kiswahili.

## 3.3 KUHUSU VIFAA VYA WALIMU NA WANAFUNZI

i) Kujua iwapo walimu na wanafunzi wanavyo vitabu vya kutosha walimu wa lugha ya Kiswahili katika shule moja iitwayo Saint Andre iliyopo mjini Kigali, walijibu ya kwamba hawana vitabu vya walimu na vitabu vya wanafunzi hawana. Ni juhudi ya Mwalimu binafsi kutafuta kitabu chochote cha Kiswahili na kokote ili waweze kusaidia wanafunzi. Njia wanayoitumia, ni mwalimu kuandika kwenye ubao na wanafunzi kunakili katika daftari zao.

Pia kuhusu vitabu vya kusomea ndani na nje ya shule havipo, na pia walimu na wanafunzi hawapati magazeti au majarida. Kwenye maktaba ya shule. Hii hudhihirisha kwamba elimu kwa upande wa Kiswahili ni shida kubwa.

ii) Swala la kupata nafasi ya kusikiliza mazungumzo ya lugha ya Kiswahili karibu walimu wote wanasikiliza matangazo ya Kiswahili kwa kupitia redio na kusikiliza idhaaa mbalimbali ulimwenguni kote wanapoongea na kutangaza kwa Kiswahili. Lakini wanafunzi hutegemea idhaa ya Taifa ya Redio ya Rwanda.

Hata hivyo si wanafunzi wengi wanaopata bahati ya kusikiliza kwenye redio au televisheni ya shule kwa kua wanafunzi wengi hupendelea taarifa ama ya lugha ya Kinyarwanda au ya Kifaransa.

iii) Swala la walimu na wanafunzi kupata nafasi ya kufanya safari za nje ya nchi walijibu kuwa haikuwezekana kwa sababu nyingi tofauti. Sababu kubwa ni ya kutokuwa na fedha za kugharamia safari pamoja na matumizi mengine kama vile kulipia vyumba vya kulala pamoja na chakula. Lakini wameona kuwa ni wazo la maana kwamba ikiwezekana wakati ujao swala hili litapelekewa wizarani ili kushughulikiwa vilivyo. Afisa mhusika wa masomo katika shule za upili aliendelea kusema kuwa nchini Rwanda kuna watu wengi

wanaozungumza Kiswahili lakini Kiswahili chenyewe kina lafudhi na lahaja mbali mbali; kama vile Kingwana, cha watu kutoka Congo, au mchanganyiko wa Kingwana na Kiswahili sanifu, kama vile Kiswahili kizungumzwacho nchini Burundi. Na lugha ya Kiswahili yenye kuchanganya Kiluganda na Kiingereza ya watu kutoka Uganda. Vile vile kuna wengine ambao huongea Kiswahili sanifu cha watu kutoka Tanzania. Kwa hivyo wakati ujao wahusika wataweza kuzingatia fikira kama hiyo.

## 3.4 KUHUSU MAZINGIRA

i) Swala la kupata wazungumzaji wa Kiswahili aidha na walimu au wanafunzi, majibu yalikuva kwamba mazingira ya lugha nchini Rwanda utakuta sana sana watu karibu wote huzungumza Kinyarwanda, lugha ambayo ni ya Taifa, hivyo ni mitaa Fulani Fulani ambako mtu anaweza kuwapata wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mitaa ya Nyamirambo, Biryogo ambako kuna Waislamu wengi. Na sehemu za soko kuu utawakuta watu mbali mbali wakazi wa jijini Kigali ambao hutoka nchi mbali mbali, kama vile Afrika ya Mashariki na ya kati na ambao ni wasemaji wa lugha ya Kiswahili.

Sehemu nyingine ni za Mikoani ambapo nchi ya Rwanda hupakana na nchi nyingine kama vile Mkoa wa Kibungo unaopakana na Tanzania, Mkoa wa Cyangugu unaopakana na Bukavu, mji ulioko mahsariki kusini ya jimbo la Kivu nchini Kongo. Sehemu nyingine

wazungumzao sana Kiswahili ni mkoa wa Kisenyi mji ambao unapakana na Goma, mji ulioko mashariki ya jimbo la Kivu kasikazini vilevile nchini Kongo.

Sehemu hizo zilizotajwa juu pamoja na maduka ya Warabu na Wahindi popote nchini, mwanafunzi au mwalimu wa lugha ya Kiswahili anaweza kuwasiliana nao bila matatizo.

ii) Madhumuni ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda, kuhusu swala hili anayehusika na uchunguzi wa ufundishaji wa Kiswahili humu nchini, alijibu kwamba Rwanda ni nchi iliyoko kanda ya maziwa makuu. Pia Rwanda ni mshirika mkuu wa nchi za Afrika ya Mashariki kwa siasa na Biashara. Hivyo itakuwa vizuri kwa mawasiliano, kwa kuwa lugha kuu ya mikutano na shughuli kadhaa za mawasiliano, kibiashara kisiasa na hata kitamaduni, kama vile nyimbo, michezo kwa mfano CECAFA n.k. huhitaji lugha kama chombo cha kuwaksilishwa mtu na mtu, au jamii na nyingine.

Kwa kuunga mkono majibu haya ya utafiti, Ireri Mbaabu (1991:113) anasema:

"...tukilinganisha vile vile hali ilivyo nchini Uganda na jirani zake Rwanda na Burundi tunaona kwamba jirani hao wameanza kukuza

Kiswahili kwa dhati. Rwanda na Burundi ambazo hutumia Kifaransa kama lugha rasmi wametambua umuhimu wa Kiswahili katika mawasiliano na ushirikiano wa kibiashara na jiriani zao wa Afrika Mashariki hasa Kenya na Tanzania"

Matokeo ya juhudi hizi yameanza kuonekana kwa kuwa wananchi wa Rwanda na Burundi wanaweza kuwasiliana na mąjirani zao wa Afrika Mashariki kwa kutumia lugha ya Kiafrika, Kiswahili…."

iii) Umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa kulinganisha na lugha nyingine za kigeni, mhojiwa alijibu kwamba kirasmi, lugha ya Kiswahili si lugha ya Taifa, lakini hali halisi si lugha ngeni. Alisema kwamba mbele ya jamii ya Wanyarwanda, Kiswahili pia ni lugha yao ya pili kwa sababu kuna jamii nyingi za Wanyarwanda zinazozungumza Kiswahili kwa maisha yao yote. Alisema kuwa Kiswahili huongewa na watu wa ngazi zote, wale waliokwenda shule na wale ambao hawakwenda shule. Hawa ambao hawakwenda shule aidha wamejifunza Kiswahili kwa kuwasiliana kimatembezi na watu wa Afrika Mashariki au na watu wa kama kutoka kwa jamii zao za Wanyarwanda kama vile wanavyojifunza lugha ya mama.

Wengine ambao wamekwenda shule hujifunza aidha shuleni au kama wale wengine waliyotajwa hapo juu. Lakini Kifaransa au Kiingereza,

mhojiwa alisema kwamba lugha hizo ni vigumu kuzifahamu bila kwenda shule na kuzisomea kwa muda wa Myaka mingi na hata watu wakirudi kutoka shule wanazisahau kwa kuwa ni lugha ambazo ni ngeni kwa Wanyarwanda. Na pia ni lugha ngumu ukizifananisha na lugha kama Kiswahili au Kinyarwanda au hata Kiganda (Kiluganda)

Tuone watu wengine wanavyotoa maoni yao kuhusu elimu ya lugha za ulaya na zile za Kiafrika. Ireri Mbaabu (1991:76) aliandika kuhusu : ubora wa Kiswahili kikilinganishwa na Kiingereza ulitiliwa makazo tena na Bwana E.G. Morris, Mkurugenzi wa Elimu nchini Uganda, , katika Ripoti ya mwaka 1932. morris aliandika yafuatayo,

"Huku inapomchukua kijana hodari mwafrika muda wa miezi sita tu kujifunza lugha ili aweze kukisoma kitabu cha Kiswahili na kukielewa barabara, ingemchukua angalau miaka sita ya kujifunza Kiingereza kwa makini ili aweze kukielewa kitabu cha Kiingereza cha kiwango sawa. Ni vigumu kuelewa vile watetezi wa Kiingereza wanavyotarajia kusitawisha elimu ya Waafrika kwa kutumia lugha ya Ulaya kama lugha ya kusomesha masomo mengine"

iv) Kwa maoni yenu Kiswahili hupendwa na wanafunzi? Swala hili wachunguzi wa lugha ya Kiswahili walitwambia kwenda kuwauliza wanafunzi wenyewe au walimu lakini hata hivyo mmoja wao amejibu kwamba bila shaka wanafunzi wanapenda lugha hiyo kwa vile wao

ndiyo wamechagua kuisomea na hakuna aliyewashurutisha kuchukua somo hilo.

Hata hivyo ilitubidi turudi kule St Andre kuuliza walimu kwa vile muda ulikuwa mdogo wa kuona wanafunzi. Taarifa ya walimu ilisema kwamba wanafunzi wengi na hata wale ambao hawachukui Kiswahili wanakipenda sana. Na hapo ndiyo wakati walipopendekeza kufundishwa wanafunzi wote lugha ya Kiswahili lakini swala hili la pendekezo bado halijajadiliwa.

v) Na swala la mwisho la kujua iwapo Wanyarwanda wanapendelea watoto wao wajifunze lugha ya Kiswahili au la.

Wahojiwa walisema kwamba siku hizi Wanyarwanda hawana imani ya kasumba kwamba Kiswahili ni lugha ya watu ambao si wasomi au kuwa kwamba ni lugha ya waislaamu, imekwisha. Walisema kwamba hivi sasa Wanyarwanda wanaelewa kuwa lugha ya Kiswahili ina umuhmu sana si kwa Wanyarwanda tu bali ulimwengu mzima.

Swali hili ni la maana kwa sababu kuna jamii ambazo zimekataa lugha ya Kigeni kutumiwa na kufundiswha makwao. Kwa mfano nchini Uganda, Ireri Mbaabu (1991:2) anaandika kwamba Waganda walianza kukipinga Kiwahili nchini humo kuanzia mwaka 1998 wakati Kabaka Mwanga (mwanawe Mutesa)

alipomwandikia Balozi wa Uingereza huko Zanzibar akilalamika kwamba Waarabu walikuwa wamedanganya kwamba Uigereza ilitaka kuigawanya Buganda kuwa koloni yao Kabaka aliwaalika Waingereza kwenda kuishi Uganda. Wabaganda ambao tayari walikuwa wameshika dini ya Kikristo walianza kupinga waarabu na dini yao ya Kiislamu pamoja na Kiswahili ambacho walikitambua kuwa chombo cha kueneza Uislamu.

Swala kama hili la kuikataa lugha ya Kiswahili si Uganda tu peke yake hata nchini Kongo wakati wa ukoloni wa Wabelgiji kumekuweko tatizo kama hili, kama vile mswada wa Rocha Chimerah (2001) unavyoandikwa;

"kuona hivyo,

Wabelgiji wakaamua kukitukuza Kiswahili (lahaja ya Kingwana) ambacho walikiona ni chombo suluhu, kwa vile hakina wasemaji wake wa kikabila, hata ijapo kilisemwa na baadhi ya watu wengi humo nchini mashariki, kaskazini mashariki na kusini mashariki.

Uamuzi huu wa wakokoni ukapingwa na wenyeji wa nchi hiyo, hasa wale wanaotoka katika makabila makubwa makubwa ya Luba, Ngala na Kongo. Hawa walidai ya kwamba Kiswahili hakina haki nchini Kongo kwa sababu si lugha ya wenyeji wa nchi hiyo bali ni lugha ya watu wa Afrika ya Mashariki"

Kinyume chake jamii ya Wanyarwanda wameshaelewa kwamba lugha ya Kiswahili ina umuhimu kwao pamoja na watoto wao kwa hivyo hawanabudi

kufurahia wakiona Kiswahili ni baadhi ya masomo yanayotolewa kwa kufundishia. Kama tume ya elimu ya Kenya (tume ya Ominde) inavyotoa maoni yake kuhusu Kiswahili (Chiraghdin 1997:7).

"...Wote waliotoa maoni walikuwa na rai sawa kuwa matumizi ya Kiswahili yapanuliwe kwa sababu moja tu ya kupatikana chombo cha ziada ambacho hasa ni cha Kiafrika cha kuungamanisha na kuleta umoja bali pia kutilia nguvu mawasiliano baina ya mataifa humu humu Afrika ya Mashariki na vile vile sehemu za mashariki ya Kongo (Zaire) na sehemu za Afrika ya kati. Basi Kiswahili kinatambulikana kuwa kina athari ya kuliunga taifa na kuwa ni njia ya mawasiliano ya umoja wa Kiafrika katika sehemu kubwa ya bara hili (la Afrika). Kwa ajili ya shughuli hizi muhimu tunaitakidi kuwa Kiswahili kiwe ni somo la lazima katika shule za msingi...kuanzia kiwango cha chini kabisa kama vitakavyowezekana."

Hivi ni wazi kwamba lugha ya Kiswahili inapendwa na kuzungumzwa na jamii ya Wanyarwanda licha ya matatizo yanayoitinga katika elimu nchini.

# SURA YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tulichunguza hali ya Kiswahili katika elimu na kupendekeza mambo kadhaa. Tulichunguza Kiswahili Rwanda kwamba hakijaendelezwa kama ilivyotarajiwa katika elimu. Pia somo letu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza sababu zinazoathiri uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika elimu nchini. Kwa mfano tulikuta kwamba walimu wenye ujuzi wa lugha ya Kiswahili ni haba. Na kwamba hakuna vifaa maalum vya kusomeshea wanafunzi shuleni na matatizo mengine mengi kama ilivyoripotiwa ndani ya utafiti. Katika utafiti, tulipendekeza hatua za kufuata nazo ni kama zifuatazo;

- Kiswahili kifundishwe tangu darasa la tatu shule za msingi na kutahiniwa au bila kutahiniwa.
- Kiswahili kifundishwe katika shule zote za upili na kutahiniwa.
- Wizara ya elimu inafaa kuandaa walimu wenye ujuzi pamoja na vifaa vya kutosheleza ufundishaji bora wa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo katika utafiti huu tumekusanya mapendekezo kutoka idara tofauti kuhusu ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo;

Pendekezo la kwanza ni kutoka Taasisi ya ukuzaji Mitaala

Hawa walipendekeza mambo kadhaa kuhusu matamanio yao ya elimu ili wapate urekebisho mzuri, kwa uchache ni haya yafuatayo;

## 4.2 PENDEKEZO LA KWANZA

(i) Walipendekeza kwamba Kiswahili kifundishwe tangu kidato cha pili kama ilivyokuwa kabla ya mwaka 1994. Walisema kwamba hii inaweza kusaidia wanafunzi kukifahamu vizuzi kiswahili kwa sababu wanafunzi watakuwa wamepata muda wa kutosha kujifunza na kujiandaa kwa mitihani ya kidato cha sita na kwendelea katika vyuo vikuu.

(ii) Wanafunzi wa vyuo vikuu vya ualimu, TTC wafundishwe somo la Kiswahili ili baadaye waweze kusaidia kufundisha na kuanzisha Kiswahili katika shule za msingi.

(iii) Walisema kuwa zamani kulikuwa na uhusiano kati ya idara ya Kiswahili nchini Rwanda na KKA (Kenya Kiswahili Association) wahusika wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala waliomba uhusiano huu urudi. Pia wangependa uhusiano kati ya chuo kikuu cha Egerton na idara ya Kiswahili aidha na vyuo vikuu nchini Rwanda au na Idara ya ukuzaji Mitaala nchini.

(iv) Walipendekeza pia kuwepo vifaa vya kutosha vya kusomesha Kiswahili .

(v) Wizara ya Elimu itayarishe kongamano za kimataifa au za kimaeneo nchini Rwanda ili kujadili juu ya mada mbalimbali za lugha ya Kiswahili.

(vi) Pendekezo la mwisho kutoka kwa wahusika wa Taasisi ya Ukuzaji mitaala walishukuru kwa kuanzisha utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili na kupendekeza utafiti zaidi katika nyanja hii.

## 4.3 PENDEKEZO LA PILI

Pendekezo hili ni kutoka kwa walimu wa shule ya upili ya Saint Andre Mjini KIGALI tulipowaona walimu hawa, majadiliano yetu na wao yalitoa majibu ambayo yalifanana na yale ya wahusika wa Taasisi ya ukuzaji Mitaala karibu yote isipokuwa kidogo tu.

Mapendekezo ya walimu yalikuwa kama ifuatavyo;

i) Walimu wapate mafunzo ya mara kwa mara kwa kujiendeleza kuhusu lugha ya Kiswahili.

ii) Walimu na wanafunzi wangepata safari kwa ajili ya mafunzo kwa mfano kwenda Tanzania ambako wanapakana karibu na Rwanda.

iii) Shule zipate vitabu vya walimu na wanafunzi; na pia wanunuliwe gazeti la Kiswahili kutoka aidha Tanzania au Kenya. Hii itawasaidia kupata mwanga kuhusu yasemwayo magazetini kwa lugha ya Kiswahili.

Pia walisema wangependa kuwa na vifaa tofauti vya kufundishia lugha ya Kiswahili kama vile kaseti video n.k.

iv) Kufanya mpango wa kuvifasiri kwa Kiswahili vitabu vizuri vya Kinyarwanda au vya Kifaransa na Kiingereza.

v) Kuwapa motisha na uwezo wale wenye uwezo wa kuandika vitabu kwa lugha ya Kiswahili.

Haya ndiyo baadhi ya mapendekezo kutoka kwa wachunguzi wa ufundishaji wa Kiswahili shule za upili pamoja na baadhi ya walimu wao.

## 4.4 HITIMISHO.

Katika sura hii, tumechunguza athari zinazotinga uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda. Tuliweza kuona kwamba mengi ya yale tuliofikilia kabla ya utafiti ni ya kweli japo yapo si yote ya kweli.

Tulijionea kwamba kuna upungufu mkubwa katika mandalizi na mafunzo ya lugha ya Kiswahili sana sana kwa upande wa walimu na kwa upande wa matini ambalo ni jambo muhimu katika mafunzo ya somo lolote. Kwamba bila kuwa na vitabu vinavyofaa au walimu wenye ujuzi huchangia kwa kutoendelea kiutaalamu katika elimu yoyote kila mahali uendapo. Hata hivyo wahojiwa walieleza kuwa lugha ya Kiswahili katika elimu nchin; Rwanda si duni kama makisio yetu yalivyobainisha. Walisema kuwa wanafunzi humaliza kidato cha sita wakiwa na uwezo wa kuandika, kusoma, kusikiliza na kuongea Kiswahili kwa wastani.

"Sisemi kwamba wanafunzi wetu wanalingana na wale wa Afrika Mashariki" Mwalimu mmoja alijitetea. Ni kweli kwamba somo la Kiswahili likipewa vifaa vya kutosha pamoja na kusomeshwa kwa muda wa kutosha wanafunzi wanaweza, nchini Rwanda, kuwa kama wale wengine ambao ni wenyeji wa lugha ya Kiswahili.

# KIAMBATISHO

## MWONGOZO WA MASWALI YA UTAFITI

KUHUSU SERA YA UFUNDISHAJI WA LUGHA YA KISWAHILI

i) Kiswahili husomeshwa kuanzia darasa gani?

ii) Ni masaa mangapi au vipindi vingapi vinavyotengewa lugha ya Kiswahili kwa juma moja?

iii) Ni lugha zipi nyingine ambazo hufunzwa katika elimu nchini Rwanda?

iv) Je, lugha nyingine hupewa masaa mangapi kwa wiki?

v) Je, lugha ya Kiswahili inatahimiwa au vipi?

vi) Je, mitihani wanayopewa wanafunzi ni rahisi, migumu, au vipi?

vii) Je wanafunzi hutegemea mwalimu kila wakati kutatua matatizo yao yote ya lugha?

## KUHUSU WALIMU WA LUGHA YA KISWAHILI

i) Kuna walimu wa kutosha wa kufundisha Kiswahili katika shule za upili?

ii) Walimu wenu wana ujuzi gani?

iii) Walimu hao walipata mafunzo wapi?

iv) Walimu hawa wanaongea Kiswahili sanifu au Kingwana?

v) Je, walimu wa Kiswahili wanapata mafunzo mara kwa mara au katika semina moja moja tu?

## KUHUSU VIFAA VYA WALIMU NA WANAFUNZI

i) Je, wanafunzi wanapata vitabu vya kusoma wakiwa nje ya shule?

ii) Walimu na wanafunzi hupata magazeti ya lugha ya Kiswahili?

iii) Je, tatizo la vitabu ni kubwa au dogo?

iv) Kuuliza iwapo wanapata nafasi ya kusikiliza mazungumzo ama hotuba kutoka kwa watu au kupitia redio au Runinga.

v) Je, walimu na wanafunzi hupata safari za mafunzo nje ya shule zao?

## KUHUSU MAZINGIRA

i) Je, walimu na wanafunzi hupata watu wa kuzungumza nao lugha ya Kiswahili?

ii) Ni nini madhumuni ya Kiswahili nchini Rwanda?

iii) Ni nini umuhimu wa Kiswahili ukilinganisha na lugha nyingine za kigeni nchini Rwanda?

iv) Kwa maoni yenu, Kiswahili hupendwa na wanafunzi wengi au wachache?

v) Je jamii ya Wanyarwanda inapenda watoto wao wajifunze Kiswahili?

## SERA YA SEREKALI

MTAZAMO WA SERIKALI (Prospective Policy)

i) Je, mnafikiri serikari ya Rwanda inapendelea Kiswahili kifundishwe kwa wingi nchini Rwanda?

ii) Je, wanafunzi hupewa kazi iwapo wamefuzu lugha ya Kiswahili?

iii) Ni nini maoni ya Serikali kuhusu lugha ya Kiswahili?

iv) Je, ni nini mtazamo wa Wanyarwanda kwa ujumla kuhusu lugha hii ya Kiswahili katika elimu nchini Rwanda?

## MAREJELEO


Barengayabo P. (1992) Matumizi ya Kiswahili nchini Rwanda; Mtazamo wa Kisimu-jamii Ruhengeri UNR

Bigirumwani Marcel, (1983) Maendeleo ya Kiswahili Nchini Burundi, TUKI, Dar es Salaam

Mtazamo wa Ruhenyeri UNR, Kl 38

Fisherman, Ja. A (1968) National Languages and Languages 0f under Communication in developing Nations in Whiteley Wlt Language use and Social change London: OUP.

Ireri Mbaabu (1991) Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili, Longman Kenya Ltd

Kavamgura J.D. (1985) Kiswahili Katika Uwanja wa Biashara nchini Rwanda:

Maznit a. (1981) Acceptibility in the planned standard: The case of Kiswahili in Kenya: Ph.D These. Standford Unviersity

Mohos. A. (1969) Language problems

Mujyambere, Hamisi S. (1983) "Maendeleo yaKiswahili Rwanda" katika TUKI

Mukama Ruth, (1983) "Hali na Hadhithi ya Kiswahili Nchini Uganda",katika TUKI

Mwasi J.D (1984) Isimu Linganishi: Makala iliyotolewa kwa matumzi ya walimu wa Ksiwahili nchini Rwanda Kigali.

Mwinyi A.H.(1970) "Madhumuni na Kazi za baraza la Taifa la Lugha ya Kiswahili", katika BAKITA

Niyibizi S. (1980) Kiswahili nchini Rwanda .Kihistoria, Isimu na Isimu Jamii Butare, UNR, Uk 189.

Ntáwigira P. (1997) Kiswahili nchini Rwanda Mchango katika Mradi wa utengenezaji wa siasa ya lugha. Butare, UNR

Ominde, H. (1964) Kenya Education Commission, Government Printer, Nairobi.

Polome, Edgar (1967) Swahili Handbook, Centre for Applied Linguistics, Washington DC.

Rocha Chimerah (2002) Kiswahili Past Present and Futrue Horizons, Nairobi University Press

Shihabuddin Chiraghdin na Mathias Mnyampala(1977) Historia ya Kiswahili Oxford University Press.

Steere, Bishop, A Handbook of the Swahili language as spoken in Zanzibar, London (1870)

Trudgil P. (1983) Sociolinguisitcs: An introduction: London Basil Blackwell

Trudgil P. (1985) Applied Sociolinguistics: London Basil Blackwell

Whitely Wlt (1968) Languages use and Social Change London OUP

______ (1971) Some factors Influencing Language Policies in Eastern Africa in Rubin J.

_______ (1973) "To plan is to choose" Published Hans Wolf Memorial lecture.

______ (1974) Language in Kenya O.U.P. Nairobi

_______ (1969) Swahili. The Rise of a National Language, Methuen and Co, Lted. London.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY